Maonyesho ya mavazi ya Swahili Fashion Week & Awards 2019 yazinduliwa rasmi.

Yanatarajiwa kufanyika mnamo tarehe 6,7 & 8 Desemba.

Wabunifu 34 kuonyesha vipaji vyao kwenye jukwaa hilo.

Jukwaa kubwa la mavazi Afrika Mashariki na kati limepanga kufanya maonyesho yake mwezi Desemba mwaka huu. Maonyesho hayo ya 12 ya Swahili Fashion Week(#sfw2019) yanatarajiwa kufanyika kuanzia tarehe 6 hadi 8 Serena jijini Dar Es Salaam na yatakutanisha wabunifu 34 wa Afrika Mashariki na kwingineko ulimwenguni.

Ikiwa imejijengea mafanikio makubwa kwenye maonyesho yake 11 yaliyopita, jukwaa la Swahili Fashion Week bado linaongoza kwa umahiri katika tasniahii ya ubunifu wa mavazi.

Muasisi wa Swahili Fashion Week Mustafa Hassanali anamatumaini ya kuimarisha msingi wa ubora wa jukwaa hilo na kwa shauku kubwa anasema,"sio tu kwamba tumeweza kuidhihirishia dunia kwamba vipaji vya ubunifu hapa Tanzania na Afrika kwa ujumla ni vya kipekee, tumeamua kupanua wigo wa jukwaa hii kwani kwa mara ya kwanza katika jukwaa hili atapanda mbunifu wa mavazi kutoka Italia, Marta Zampolinia mbaye pia atazungumza na wabunifu na wadau mbalimbali kwenye sekta hii ya ubunifu namna ya kupanua wigo wao wa kimasoko kuwa wa kimataifa kwenye warsha itakayofanyika hivi karibuni inayoandali wanajukwaa hili.. kama usemavyo msemo wa Kiafrika, ukitaka kwenda kwa haraka, safari peke yako, lakini ukitaka kufika mbali zaidi ..ambatana na wenzako"

Mustafa anaongeza,"lengo la kuendeleza tasnia ya ubunifu Afrika bado linabaki mstari wa mbele, kwa kupitia jukwaa hili na mtandao wake mkubwa wa vyombo vya habari, watumiaji wa bidhaa za ubunifu wa Tanzania na Afrika kwa ujumla sasa wataweza kuona mbadala wa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje, wakati wote tumekua tukitilia mkazo thamani ya bidhaa za ubunifu za Afrika kwa kuhamamish adhana ya "made in Africa" nakutengeneza bidhaa zenye hadhi ya kimataifa kwa misingi ya Kiafrika.

Maonyesho haya ya 12 bado yataendelea kuwa mwanga wa maonesho mengine ya mavazi Afrika kwa wabunifu wa Kitanzania, ukanda wa Afrika Mashariki hata wale wa kimataifa kwa mvuto na mandhari yake ya kipeke

“Tunauhamasisha umma wa Watanzania kupenda kuvaa mavazi yaliyobuniwa na wabunifu wa hapa Tanzania (Made in Tanzania). Kwa kufanya hivyo tunakuza vipaji vyao na kuwafanya siku moja kutambulika kama wabunifu wakubwa Ulimwenguni. Upendo unaanzia nyumbani na ndiyo dhumuni ya kufanya haya..kukuza tasnia hii ya ubunifu”Aliongeza Hassanali.

Katika Maonyesho ya mwaka huu pamoja na maonyesho ya mavazi(runway) yatakayofanyika kila siku kwa kipindi cha siku tatu mfululizo kuanzia saa 2.30 usiku, kutakua na Bazaar ambapo wabunifu wataonyesha na kuuza bidhaa zao mbalimbali. Sambamba na hilo tutasheherekea na kutambua mchango wa wadau mbalimbali kwenye tasnia ya ubunifu ambapo tuzo kutoka vipengele 26 zitatolewa. “Mwaka huu tumeongeza kipengele kipya kwenye tuzo zetu Mbunifu wa Mwaka (mikoani) ambapo tutaangalia wabunifu waishio na kufanya kazi zao mikoa mingine tofauti na Dar Es Salaam ilikuzifanya tuzo zenye kushirikisha wadau wengi zaidi. Tuzo za Swahili Fashion Week zinaletwa kwenu na Green Telecom na kusimamiwa na Nexia SJ“ alisema Hassanali.

Swahili Fashion Week & Awards 2019 imedhamiria kwenye matumizi teknolojia ya hali ya juu kwa kuonyesha umahiri wa uandaaji katika kipindi cha siku hizo za mitindo na urembo, pamoja na miondoko ya wanamitindo waliojiandaa vizuri jambo litakaloendelea kuiweka Tanzania kwenye kilele cha ubora. Tanzania, Haisahauliki (Tanzania, Unforgetable).

Swahili Fashion Week Inaandaliwa na kuratibiwana 361 Degrees Africa Ltd, wenyeji wakiwa ni Hoteli ya Serena Dar Es Salaam na inadhaminiwa na UbaloziWa Italia Tanzania, Grey Goose, Hugo Domingo, Image Masters, Asila’s Make Up, Nexia SJ, Green Telecom, Epidor, Events lites, Michuzi Blog , Fashion Association of Tanzania pamoja na Baraza La Sanaa La Taifa(BASATA).

Wabunifu katika jukwaa la mwaka huu ni:
SHAHBAAZ SAYED | CHUWA FASHION | BY JV's | KISUSI DESIGNS | MKWANDULESON |

DOREEN MASHIKA | BIJOUX TRENDY | LUNDI & SONS | MK | MILLYZ | KIKI'S | NALEDI |
LUCKY CREATIONS | NESTE | EK AN TIK | ANNA SEMIONO | CHARLES ENNO | NISHIKEMKONO ORG | LEVRA WITH CULTURE | AM DESIGNS | MAHAUMMES |
TUNTIFADY | GLORY MISSANA | NASHAKI | SAMZ | NUCY | PALSE | AFRIKAWALA |
MARY ANGEL | RUFFIN | CLAVON LEONARD | MARGAUX RUSITA | BERYL QOUTURE |
SAMMA COLLECTIONS | MARTA ZAMPOLINI | UWERA CLAUDINE.

Kuhusu Swahili Fashion Week:
Swahili Fashion Week Ni Jukwaa kubwa la maonyesho ya mavazi Afrika Mashariki na kati linalotoa fursa kwa wabunifu wa mavazi kutoka nchi zinazozungumza lugha ya Kiswahili na kwingineko Afrika kuonesha vipaji vyao nakupanua wigo wao wa masoko. Dhamira kuu ni kudhihirisha kwamba ubunifu wa mavazi ni shughuli inayoweza kumwingizia mtu kipato sambamba na kuhamamisha dhana ya Made in Africa.
Maonyesho ya Swahili Fashion Week yalianzishwa mwaka 2008 na muasisi wake Mustafa Hassanali.
Mwaka huu wa 2019 yakiwa ni maonyesho yake ya 12.

Maulizo kwa Vyombo vya habari, Wasiliana na Nzonesta +255 784 967324

Barua Pepe:
info@swahilifashionweek.com